

# TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA (TCU)



## TAARIFA KWA UMMA

### MUDA WA KUTHIBITISHA UDAHILI KWA WALIODAHILIWA ZAIDI YA CHUO KIMOJA MWAKA WA MASOMO 2019/2020

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inapenda kuutangazia Umma kuwa muda wa kuthibitisha udahili kwa waombaji waliodahiliwa chuo zaidi ya kimoja katika awamu ya kwanza ya udahili mwaka wa masomo 2019/2020 utamalizika siku ya Alhamisi, tarehe **29 Agosti, 2019** saa sita usiku.

Mpaka sasa zaidi ya waombaji 16,000 sawa na asilimia 77 ya waliokuwa na udahili zaidi ya chuo kimoja wameshajithibitisha. Tume inapenda kuwatoa hofu waombaji ambao bado hawajakamilisha uthibitisho kuwa hakuna mtu atakayekosa udahili kwa sababu ya kushindwa kujithibitisha. Kwa kuzingatia hilo kutakuwa na awamu tatu za kuthibitisha udahili kwa wale waliodahiliwa zaidi ya chuo kimoja kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 1.

#### Jedwali 1: Utaratibu wa Kuthibitisha Udahili

Awamu	Muda	Wahusika
1.	20-29 Agosti 2019	- Waliodahiliwa zaidi ya chuo kimoja awamu ya Kwanza.
2.	8-13 Septemba 2019	- Waliodahiliwa zaidi ya chuo kimoja awamu ya Pili; na - Walioshindwa kujithibitisha katika awamu ya kwanza kutokana na sababu mbalimbali.
3.	21-30 Septemba 2019	- Waliodahiliwa zaidi ya chuo kimoja awamu ya Tatu; na - Walioshindwa kujithibitisha katika awamu ya kwanza na awamu ya pili kutokana na sababu mbalimbali.

Tume inaendelea kuwasisitiza waombaji waliodahiliwa zaidi ya chuo kimoja ambao bado hawajajithibitisha wathibitisha vyuo wanavyopenda kusoma mapema iwezekanavyo ili kuondoa usumbufu usiokuwa wa lazima. Kwa wale ambao wanachangamoto katika kujithibitisha, vyuo vyote vimeelekezwa kupokea taarifa zao na kutafuta ufumbuzi wa haraka kwa kuzingatia miongozo na taratibu zilizowekwa. Hivyo waombaji wote watakaoshindwa kujithibitisha wanashauriwa kuwasiliana na vyuo husika, ili wapokee taarifa zao na kuzifanyia kazi.

Ifahamike kuwa maombi ya udahili na kujithibitisha yanafanyika kupitia akaunti za vyuo ambazo waombaji walizitumia wakati wa kuomba udahili.

Tume itaendelea kutoa taarifa kadri zoezi la udahili litakavyokuwa linaendelea.

Imetolewa na:



Prof. Charles D. Kihampa  
**Katibu Mtendaji**  
**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania**

**28/08/2019**